

More past papers are available on <http://www.kenyaplex.com>

Kenyatta university Ect 313 Past Paper

Jibu maswali MATATU tu.maswali yote yateuliwe kutoka kila sehemu.

Swali LA KWANZA ni lazima.

SEHEMU A. UFUNDISHAJI WA LUGHA.

1 a.Eleza namna sifa za lugha zifuatazo zinavyoweza kukufaa katika kufundisha madam za kiswahili.

-sauti za lugha ni za kutamkwa.

-lugha hufungamana na utamaduni wa jamii

b.Eleza jinsi unavyoweza kutumia nadharia ya maigizo na vitendo kufundisha vitenzi.

c.Eleza jinsi unavyoweza kufundisha madam yoyote ya lugha kwa kurejelea stadium zote za lugha.

d.Fafanua mbinu zozote nne unazoweza kufundisha sajili mbalimbali za lugha.

SEHEMU YA B. UFUNDISHAJI WA FASIHI

2 a."Methali zinaweza kutumiwa kuendeleza lugha na utamaduni wa jamii"

-Eleza namna unavyoweza kutumia methali ifuatayo kukuza lugha na ufahamu wa utamaduni wa jamii.mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

-Eleza namna unavyoweza kufundishia methali hiyi

b.Kwa kutoa mifano,eleza jinsi unavyoweza kuwasaidia wanafunzi wako kuelewa dhana ya Uhuru wa kishairi.

3.Kwa kurejelea riwaya ya Kidagaa kimemwozea (ken walibora).Eleza namna unavyoweza kuwasaidia wako kuelewa mbinu za lugha katika riwaya

SEHEMU YA C. MAANDALIZI YA MWALIMU

4.Lengo lako mi kuangazia mhusika mkuu katika Tamthilia ya Mstahiki Mega(Timothy Arege)

a. Andika madhumuni matatu yanayolenga kufanikisha somo hili.

b.Eleza jinsi utakavyo fanikisha madhumuni yako huku ukionyesha shughuli za kushirikisha wanafunzi wako katika sehemu zifuatazo;

-Utangulizi

-Mwendelezo wa soma

-Hitimisho

5.Eleza mambo matano ya kimsingi ambayo mwalimu anapaswa kutilia maanani anapotunga maswali ya kutathmini uelewa wa makala ya ufahamu